

# HALMASHAURI YA WILAYA MWANGA

(Barua zote zianzikwe kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji)

## MKOA WA KILIMANJARO

Simu Na: 027 2974343

: 027 2974344

E-Mail [ded@mwangadc.go.tz](mailto:ded@mwangadc.go.tz)

Web site: [www.mwangadc.go.tz](http://www.mwangadc.go.tz)



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P. 176

MWANGA

Unapojuji tafadhali taja:

Kumb. Na. L.10/7/A/40

23 May, 2022

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga imepokea kibali cha ajira chenye kumb. Na. FA.97/228/01/9 cha tarehe 13/05/2022 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hivyo, natangaza nafasi za kazi kwa watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ifuatayo:-

## MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III – NAFASI 7

**SIFA:** Mwenye Elimu ya Kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo:-

Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii au Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

### MAJUKUMU.

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa mlnzi wa amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- v. Kutafisiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati au kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaaluma katika kijiji
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za vijiji.

### NGAZI YA MSHAHARA

Mshahara ni kwa mujibu wa viwango vya mishahara Serikali yaani TGS B.

## KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III – NAFASI 4

**SIFA:** Mwenye Elimu ya Kidato cha nne (IV) aliyehitimu mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya tatu. Wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kingeeza maneno 80 kwa Dk. Moja na wawe wamepata mafunzo ya kopmyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Window, Microsoft Office, Internet, Email na Publisher.

### **MASHARTI YA JUMLA**

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.
2. Mwombaji awe na umri unaoanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45 na awe na hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
3. Maombi yote, waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitokeza (Detailed C.V)
4. Maombi yote ya waombaji yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu kidato cha IV, cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (passport size) na iandikwe jina nyuma.
5. "testimonials, Provisionala Results, Statement of Results" hati ya matokeo ya kidato cha nne au sita (FORM IV AND FORM VU RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.
6. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wakikishe vyeti vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika TCU na NECTA na taarifa ya Uhakika iambatanishwe kwenye maombi.
7. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa UMMA hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wanakibali cha **KATIBU MKUU Kiongozi**
8. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi watusika watachukuliwa hatua za kisheria. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 06/06/2022 saa 9:30 alasiri
9. Taarifa nyingine muhimu tembelea tovuti ya Halmashauri [www.mwangadc.go.tz](http://www.mwangadc.go.tz)
10. Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA,  
S.L.P 176,

  
Mwajuma A. Nasoga  
Mkurugenzi Mtendaji  
MWANGA. YA MWANGA

Nakala: Katibu Mkuu,  
Ofisi ya Rais,  
Sekretarieti ya Ajira,  
S.L.P 63100,  
**DAR ES SALAAM.**